


3. اللسان Al-lisaan - Ulimi.

Katika ulimi kuna makhaarij manne makuu na ndani yake hupatikana makhaarij kumi kwa uchambuzi.

i	Mbali ya ulimi (mwishoni karibu na koo)	أَفْصَى اللِّسَانِ (مِمَّا يَلِيهِ الْحَلْق) Aqswal-lisaani (mimmaa yalil-halq)
ii	Katikati ya ulimi	وَسَطُ اللِّسَانِ Waswatwul-lisaan
iii	Sehemu ya ncha ya ulimi	طَرَفُ اللِّسَانِ Twaraful-lisaan
iv	Pembeazoni mwa ulimi	حَاقَّةُ اللِّسَانِ Haafatul-lisaan

Matokeo makuu ya herufi katika ulimi



Tanbihi: رَأْسُ اللِّسَانِ Ra-asul-lisaan (ncha ya ulimi) inajumuika na طَرَفُ اللِّسَانِ (sehemu ya ncha ya ulimi).

i- أَقْصَى اللِّسَانِ Aqswal-lisaani - Mbali ya ulimi (mwishoni karibu na koo)

Kuna makhraj mbili:

- a) Makhraj ya ق ambayo hutoka sehemu iliyopo shinani (mwisho) kabisa ya ulimi karibu na koo panapokutana na sehemu ya juu ya kidakatonge (kilimi)
- b) Makhraj ya ك iko nyuma ya ulimi lakini sio nyuma kabisa kama inapotoka makhraj ya ق bali mbele yake kidogo kwa kukutana na sehemu ya juu ya kinywa (kaakaa)

ii- وَسَطُ اللِّسَانِ Waswatwul-lisaan – Katikati ya ulimi

Kuna makhraj moja tu inayotoa herufi tatu nazo ni ¹ ي ش ج. Herufi ya ي inayotoka katika makhraj hii ni ile isiyokuwa ya madd, na inapotoka njia yake huwa haifungiki bali inakuwa wazi kidogo.

Herufi ya ج hutoka kwa kuunganika kikamilifu baina ya katikati ya ulimi na sehemu inayokabiliana nayo ya kaakaa la juu, na wakati huo huo huwa ukingoni mwa ulimi katika chonge² za chini. Inapoanza kutoka njia yake ya kutokea huwa imefungika kisha inapotamkwa huwa wazi.

Herufi ya ش inatoka katika makhraj hii ikiwa iko wazi yaani haifungiki njia yake ya kutokea, bali njia yake inafinyika tu lakini inabakia wazi.

iii- طَرْفُ اللِّسَانِ Twaraful-lisaan -Sehemu ya ncha ya ulimi :

¹ Herufi zote hizi zemekusanyika katika neno la kiarabu: الجيش. Na herufi hizi huitwa na kueleweka kama ni herufi za shajariyyah kwa kuwa zinatoka atika shajar (mti) wa mdomo nao ni baina ya katikati ya ulimi na kinachokabiliana nao miongoni mwa taya za juu.

² Meno makali yenye ncha.

Kuna makhaarij matano:

- a) Sehemu ya ncha ya ulimi pamoja na ufizi wa meno ya mbele yaliyoko juu, inatoka herufi ya ن ; herufi hii katika utokaji wake huwa iko karibu kidogo na makhraj ya ج kwa ndani kidogo zaidi; pamoja na kushirikishwa na pua (khayshuwm).
- b) Sehemu ya ncha ya ulimi pamoja na ufizi wa meno ya mbele yaliyoko juu inatoka herufi ya ر . Herufi hii katika utokaji wake huwa iko nyuma ya makhraj ya ن kwa ndani kidogo zaidi na ulimi hukunjika kwa pande zote mbili.
- c) Sehemu ya ncha ya ulimi pamoja na mashina ya juu ya ufizi wa meno ya mbele yaliyoko juu zinatoka herufi za ت د ط
- d) Sehemu ya ncha ya ulimi pamoja na ukingo wa ufizi wa meno ya mbele yaliyoko chini zinatoka herufi za ز س ص
- e) Sehemu ya ncha ya ulimi pamoja na ukingo wa meno ya mbele yaliyoko juu zinatoka herufi za ث ذ ظ Hizi zinajulikana kama ni 'Herufi za meno'

iv- حَافَّةُ اللِّسَانِ Haaffatul-lisaan – Pembezoni mwa Ulimi (kote kuwili: kulia na kushoto)

Kuna makhraj mbili:

- a) Makhraj ya ض³ ambayo hutoka katika pande zote mbili za pembezoni mwa ulimi zinapogusana na mizizi ya magego. Pande mbili hizi hushirikiana na 'Sehemu ya ncha ya ulimi' kuitamka herufi ya ض, lakini herufi inatoka zaidi kwa nguvu na inathibitika kutokana na 'Pembezoni mwa Ulimi'.

³ Ni herufi inayopatikana katika lugha ya Kiarabu pekee na ndio ikajulikana kwa *Lughatudhw-Dhwaad* (lugha ya ض)

- b)** Makhraj ya ج hutoka katika ‘Pembezoni mwa Ulimi’ kwa kushirikiana na ‘Sehemu ya ncha ya ulimi’ pamoja na kugusana na ufizi wa meno ya mbele ya juu. Herufi hii inaenea sehemu nyingi za kinywa.